



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI  
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



**TAARIFA KWA UMMA**

**KUENDELEA KUPATIKANA KWA HUDUMA ZA TEKSI MTANDAO NCHINI**

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), kwa mujibu wa Sheria Na. 3 ya mwaka 2019 ilitangaza viwango vya nauli za teksi mtandao kupitia Gazeti la Serikali Na. 1369 la tarehe 8 Aprili, 2022 na vyombo vingine vya habari.

Pamoja na viwango vya nauli za teksi mtandao, Mamlaka iliweka kiasi cha ukomo wa makato ya asilimia 15 kutoka katika mapato ya dereva kwenda kampuni za teksi mtandao kama kamisheni. Hata hivyo, baadhi ya kampuni za teksi mtandao zilizokuwa zikitoza kamisheni ya asilimia 20 mpaka 31 hazikuridhika na kiwango elekezi cha asilimia 15.

Kampuni zingine za teksi mtandao zikiwemo **InDrive, Little Ride, Paisha na Ping**, zimeridhia na zinaendelea kutoa huduma kwa viwango vya nauli na kamisheni vilivyoidhinishwa na Mamlaka.

Aidha, Mamlaka imepokea taarifa ya kampuni ya Bolt ikieleza nia ya kusitisha huduma za usafiri wa magari yanayopokea pesa taslim kuanzia tarehe 17 Agosti, 2022.

Mamlaka inawashauri abiria na madereva wa teksi mtandao kuwa, wakati inaendelea kushughulikia changamoto za huduma za teksi mtandao, waendeleo kutumia huduma za teksi mtandao zinazotolewa na kampuni zilizoainishwa hapo juu.

**Imetolewa na;**

**Kitengo cha Mawasiliano  
16 Agosti, 2022**

